# LEARNING BY EAR 2012

## ““Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”
’

## EPISODE 3: ‘Nini kilichotokea?’

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: PATO AND BOMBA MEET IN THE FIELD**

- **Pato (f, 16)**
- **Bomba (m, 18)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: DULU FINDS HIS WIFE BESIDES THE WATERHOLE**

- **Dulu (m, 40)**
- **Nuru (f, 30)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE THREE: JUDY GIVES A PRESS CONFERENCE ON THE REBELS' RAPING SPREE

- **Judy (f, 40)**
- **3-4 Journalists (age and sex not important)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE FOUR: PATO IN BIOLOGY CLASS WITH MR. MANENO

- **Pato (f, 16)**
- **Maneno (m, 45)**
- **5-7 boys and girls (15-16)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**UTANGULIZI:**

Salam kemkem tukikuribisha katika kipindi hiki cha **Noa bongo- Jenga maisha yako'**. Hiki ni kipindi cha tatu katika hadithi iitwayo **"Wasaliti walo karibu '.** Ikiwa unasikiliza kipindi hiki kwa mara ya kwanza, tutakujuza mchakamchaka mambo yalivyokuwa. Nuru, mke wa Dulu mwenye mimba changa, alinajisiwa kinyama alipokuwa kisimani akiteka maji kufaidi aila yake. Kwengineko, Allan, mtoto wa miaka kumi, ashaanza kuteswa kimwili na mpenzi wa mamake ambaye hana huruma naye, tayari keshamtandika na kumtishia maisha iwapo Allan atamwambia mamake. Na katika shule ya mseto ya bweni, Pato mwenye miaka 16, anaduwazwa na maongezi yake na mwalimu msimamizi wa mabweni, Bw.Maneno. Manenno amemtunuku godoro jipya, lakini alimwambia aweke siri hiyo. Ni bayana Bw. Maneno alikuwa anapiga mluzi na hayuko mbali kuimba, analo alilo nalo. Endelea kusikiliza ujue mbivu na mbichi katika kipindi hiki cha leo, kwa jina **'Nini kilichotokea?'** Pato amemaliza majuma sasa shuleni. Ni mwanariadha makini, na daima anadamka asubuhi kwenda mazoezini. Leo anapatana na Bomba, mwanafunzi wa zamani hapo shuleni.

**SCENE ONE: PATO NA BOMBA UWANJANI**

1. **SFX: MORNING ATMO**

2. **PATO:** **(doing some stretching exercises)** Moja - mbili… moja - mbili… moja - mbili… **(takes deep breath)** Sawa… sasa twende mizunguko kumi uwanja mzima. **(Pato acts as if jogging lightly)**

3. **SFX: PATO JOGGING; BOMBA JOINING HER**

4. **BOMBA:** **(jogging lightly)** Vipi kichuna… wewe… tafadhali, samahani kidogo… wewe ni mgeni hapa, sivyo? Sijawahi kukuona hapo kabla.

5. **PATO:** **(keeps jogging, breathing heavily)**

6. **BOMBA:** **(jogging along)** Naitwa Bomba. Mimi ndiye kinara wa timu ya wanariadha hapa shuleni. Nimekuona kwa muda sasa. Wewe ni mwanariadha mzuri.

7. **PATO:** **(stops and pauses)** Sawa, nimesikia, kuna la ziada?

8. **BOMBA:** **(caught off guard)** Mimi? Sawa… hamna, kwa kweli. nilikuwa… nilikuwa…

9. **PATO:** Sasa, ni hivi, unanitia uvivu wa mazoezi na kunipotezea muda. Kwaheri.

10. **BOMBA:** **(laughs out loud)** Unanichekesha. Yani una maanisha unayoyasema, kweli? … unajua ni wasichana wangapi wanatamani kuzungumza na mimi?

11. **PATO:** Hamna shida, waite waje wakuongeleshe. **(starts jogging again)**

12. **BOMBA:** **(shouts after PATO)** Ngoja! Unaitwaje vile?

13. **PATO:** **(while jogging away)** Huna haja ya kujua jina langu. Nafikiri majina unayoyajua yanakutosha.

14. **BOMBA:** **(thinking aloud)** Hmm… Sawa, sasa unajifanya mgumu kupatikana. Lakini haijalishi, tutakwenda juu chini lazima nitakupata tu… **(laughs, but not in a malicious way)**

15. **MSIMULIZI:** Pato ni mrembo, na mwerevu. Ni mahiri katika riadha, lakini mbele zaidi anatafakari masomo yake. Anaendelea na mbio zake, anamuacha Bomba akiduwaa, na anakwenda kujiandaa kwa darasa lake. Laita angelijua kuwa kuna mtu anamtazama kule kiwanjani akiongea na Bomba, Bw. Maneno, mwenye macho ya mwewe, kasimama dirishani mwake anafuatilia nyendo zote. Alipomuona Pato na Bomba, alijuwa ni lazima achukue hatua… lakini kabla kuangazia ni hatua ipi aliyochukua, turudi kule kisimani, wakati giza limeshamiri na Dulu anapasua kiza hicho na mwanga wakurunzi aliyoshika mkononi, akimtafuta mkewe, Nuru.

**SCENE TWO: DULU AMPATA MKEWE KANDO YA KISIMA**

16. **SFX: NIGHT ATMO IN FOREST**

17. **DULU:** **(calling out)** Nuruuu!... Nuruuu! Nu-- **(shocked by what he sees)** Oh Mungu wangu! Hapana! *Nuru…*

18. **SFX: TORCH FALLS TO THE GROUND**

**19. DULU:** **(breaking down)** Wamekufanya nini…? La! hapana… Nuru, amka… hebu fungua macho yako… ni mimi, Dulu, mimi mume wako… tafadhali, mpenzi wangu – hebu fungua macho yako…

**20. NURU:** **(regaining consciousness, moaning with pain)** Arrgh… mimi… arrgh… oh… nisaidie...

**21. DULU:** **(excited)** Nuru! U mzima! Oh, mpenzi wangu, nafurahi unazungumza… sawa, tulia. Niko hapa; nitakupeleka hospitali, utahudumiwa nikiwa hapo, usihofie.... na huyo mnyama aliyekutendea haya … **(bitterly)** nitamuwinda na nimuue!!

**22. MSIMULIZI:** Kadri alivyomuona mkewe kwenye hali ile ya unyonge na kudhulumiwa ndivyo Dulu alivyohisi uchungu, mithili ya kisu kikiunyanyua moyo wake, huku akijawa na hasira na uchungu. Lakini anajikakamua hisia zisimzidi, anapopata nguvu, alimuinua mkewe akasimama, akamgubika mkewe na mararu yaliobakia nguoni mwake, akampeleka hospitali. Siku ilipokucha, habari nchini kuhusu wasichana na wanawake walionajisiwa na waasi hao zilienea kila pembe ya mji huo. Yule aliyeshtushwa na habari zaidi alikuwa Judy. Judy anafanya kazi na shirika moja la kibinafsi linalohamasisha watu kusimama kidete dhidi ya dhuluma hizo za ngono linaloitwa SUSV – “Stand Up to Sexual Violence”- anaposikia haya anaita waandishi wa habari kuhutubia umma.

**SCENE THREE: JUDY ANAZUNGUMZA NA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU WIMBI LA VISA VYA UBAKAJI NA WAASI**

**23. SFX: CAMERA FLASHES AND LOW MURMURS**

**24. JUDY:** Nawashukuru kwa kuja haraka licha ya wito mfupi. Ni kama mlivyosikia, kuna kundi haramu linazunguka, kuwadhalilisha na kuwanajisi wanawake. Tumeshtushwa na kusikitishwa na vitendo hivi vya kinyama, miongoni mwa vingine vinavyofanywa dhidi ya wanawake. Shirika langu limekuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanawake dhidi ya dhulma zote wanazopata hususan za kingono.

**25. Journalist 1:** Sasa, Judy, shirika lako, hivi sasa, linapanga kuchukua hatua gani?

**26. JUDY:** Kama kawaida, changamoto ni kuwafahamisha na kuwaaminisha waathiriwa kuwa msaada sasa unapatikana. Tutawasadia na kuwachukulia sheria waasi iwapo watajitokeza kuwatambua. Pia, tutawapa ushauri wa kiafya, na ushauri wa kisheria, pamoja na matibabu wale wote walioathiriwa. Vilevile, tutapanga maandamano ya amani ili kupinga unyama huu, na tunatoa wito kwa wanawake na wanaume watuunge mkono. Na tunaomba uchunguzi kamili ufanywe kuhusu maasi

haya, na hatutapumzika mpaka waasi hawa washtakiwe. Nawashukuru tena kwa kukubali wito wetu.

**27. SFX: MORE CAMERA FLASHES**

**28. MSIMULIZI**: Shirika la Judy, "**Stand Up to Sexual Violence**" linalopiga vita dhulma za kingono, lilianzishwa kwa dhamira ya kuwasaidia wote wale walioadhulumiwa kwa hali yoyote ile, kusaidia katika upelelezi wa dhulma za kingono, na pia kuwapa msaada wa kisheria na matibabu wale wasioweza kujigharamia. Kazi ngumu ikiwa ni kuwapa ushauri wathiriwa wa ubakaji wakati wenyewe hawajajikubali. Ijapokuwa hawana hatia, wengi hujilaumu wenyewe, muda mwingi hawaoni ni kwanini hayo yawatendekee wao. Shirika la Judy litapata kazi nyingi za kuwasaidia waathiriwa wa vitendo hivyo hivi sasa. Lakini kwanza turudi kwa Pato, akimaliza siku yake shuleni. Somo lake la mwisho ni la Vimelea au Baiolojia, na linafunzwa na Bw. Maneno, mkuu wa bweni.

**<u>SCENE FOUR: PATO KATIKA SOMO LA BAIOLOJIA LA BW. MANENO</u>**

**29. SFX: HIGH SCHOOL CLASSROOM ATMO**

**30. MANENO:** **(teaching)** Kwa hivyo; leo tumejifunza jinsi mamba zinavyotungwa na watoto wanavyotengenezwa.

**31. SFX: CHEEKY LAUGHTER FROM STUDENTS**

**32. MANENO:** Mbegu za uzazi hutengeneza mtoto wakati mbegu za mume zikikutana na yai la mwanamke. Kwa hivyo, wasichana kumbukeni kuwa: mnahitaji kuwa waangalifu, kwa sababu ni rahisi kwenu kupata mimba.

**33. SFX: APPLAUSE AND WHISTLES FROM BOYS**

**34. MANENO:** Na nyinyi wavulana, pia muwe na tahadhari, kwa sababu hamuko tayari kuwa mababa, kwa wakati huu.

**35. SFX: APPLAUSE FROM GIRLS THIS TIME**

**36. MANENO:** Lipi la kufurahisha hapo? Lakini kwanini kila nikifunza somo hili huwa wanafunzi wanafurahia namna hii?

**37. SFX: LAUGHTER FROM THE PUPILS**

**38. SFX: SCHOOL BELL RINGS / STUDENTS VOICES HEARD IN THE BACKGROUND**

**39. MANENO:** Tukutane tena katika somo, siku ya Jumatatu. Wale mnaokwenda nyumbani juma hili, nisalimieni wazazi wenu. Pato, tafadhali hebu subiri nyuma kidogo...

**40. SFX: DESKS AND CHAIRS BEING DRAGGED; SOUND OF CLASS LEAVING**

**41. PATO:** Ndiyo, Bw. Maneno.

**42. MANENO:** Hebu rudisha mlango. Kuna kelele sana.

**43. SFX: DOOR BEING CLOSED**

**Silence**

**44. MANENO:** Pato, ulikuja hapa shule kusoma au kukimbizana na wavulana?

**45. PATO:** **(astonished)** Mwalimu…? … Wamaanisha nini mwalimu?

**46. MANENO:** **(harshly)** Unaniona mjinga! Wewe unajua pia kuwa mimi kama mkuu wa bweni, ndimi mwalimu wa pili kwa amri hapa shule ya sekondari ya Kilindi. Mwalimu mkuu peke yake ndiye aliye juu yangu

kicheo. Nafahamu yote yanayoendelea humu shuleni.

47. **PATO:** **(confused)** Lakini mwalimu... bado sikuelewi…

48. **MANENO:** Nimekuona mkicheza uwanjani na Bomba. Mlikuwa mnafanya nini?

49. **PATO:** Hakuna! Alikuwa ananieleza kuwa yeye ndiye kinara wa timu ya riadha hapa shuleni. Na hata hivyo, sikumsikiliza kwa muda mrefu.

50. **MANENO:** Pato, kama ningelikuwa wewe, ningejiepusha sana na yule kijana. Na uwe mbali sana na yeye, matokeo ya somo lako la baiolojia hayanifurahishi kwa sasa. Masomo yote unafuzu kasoro hili tu. Lakini naweza kukusaidia upite.....

51. **PATO:** Bw. Maneno, najitahidi niwezavyo. Tafadhali niamini.

52. **MANENO:** Najuwa unafanya juhudi. Kwanini niamue kukusemesha wewe peke yako? Sikiliza, Pato. Nataka uwe wa kwanza darasani, naweza kukusaidia ufaulu hivyo. **(soft whisper)** Lakini na wewe iwapo utanisaidia.

**53. SFX: MOVEMENT OF CHAIR AS MANENO GETS UP**

**54. PATO:** **(unsure of what to do, say)** Mwalimu, unafanya nini?... Tafadhali mwalimu.... La usifanye hivyo...

**55. MANENO:** Mimi ni mwalimu wako, Pato. Siwezi kukuumiza. Siwezi kufanya lolote ovu kwako. Nataka kukutayarisha uwe mwanamke kamili. Unataka kupita somo la baiolojia, au la? Unataka kuwa wa kwanza darasani kwako? Hii ndiyo nafasi pekee, usiipoteze Pato.

**56. PATO:** Lakini…

**57. MANENO:** **(orders)** Hakuna cha lakini. Sasa, hebu keti chini, tulia, na usihofie. Hakuna atakayetupata. Ni kama nilivyokwambia, mimi ni wa pili kwa cheo shuleni humu.

**58. SFX: CHAIR BEING SLOWLY DRAGGED**

## 59. MUSIC INTERLUDE

## <u>HITIMISHO:</u>

Pato aliganda. Akili yake ikimpaa ufahamu kwa mbali, ndiyo anafahamu kuwa Bw. Maneno alikuwa akimtomasatomasa na asijuwe atatorokaje. Amekwama. Hana budi. Alifunga macho yake, na kufikiri anakimbia... mbio na mbio, akikimbia miduara baada ya miduara, akikimbia mbali, akikimbia kadri ya uwezo wake. Anapofunguwa macho yake karibu na utepe, anamkuta Bw. Maneno amekwenda zake. Lakini alijuwa jambo ovu na la aibu lishamtendekea. Shati lake imefunguliwa vifungo, sidiria imefunguliwa… Pato atayakabili vipi maasi ya mwalimu wake? Tutayang'amua hayo kipindi kijacho katika hadithi hii ya, **'Wasaliti walo karibu',** unaoangazia maasi ya dhuluma za ngono. Kumbuka, kuna Nuru aliyeko hospitali, atapona lini jeraha la kubakwa kinyama. Atakubali yaliyomtokea? Na Allan ataendelea vipi na mdhalimu Uncle Joe? Haya na mengineyo ni katika kipindi kijacho. Kama unataka kusikiliza tena kipindi hiki au kingine kilichotangulia, tembelea wavuti wetu dw.de/lbe. Au jiunge na majadiliano yetu katika mtandao wa Facebook. Mpaka kipindi kijacho tutakapokutana tena, Kwa heri.